

# Serikali kupunguza tozo usindikaji maziwa

Aurea Simtowe, Mwananchi  
asimtowe@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Serikali imesema inaangalia namma ya kupunguza utitiri wa tozo kwenye mnyororo wa thamani wa maziwa yanayozalishwa na kusindikwa nchini.

Akizungumza juzi katika mukutano wa Chama cha Wasindikaji wa Maziwa nchini (TAMPA) jijini hapa, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alisema Serikali pia itaendelea kuondoa tozo kwenye bidhaa zinazotumika kwenye uzalishaji wa maziwa nchini.

Mbali na kupunguza tozo, pia Waziri ameiagiza Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB) kushirikiana na Chama cha Wasindikaji wa Maziwa (TAMPA) kuongeza uhitaji wa maziwa kwa wananchi badala ya kuen-delea kutumia nguvu kub-

wa kusitiza uzalishaji na usindikaji wa bidhaa hiyo.

"Nimesikia malalamiko hapa kuwa yale malori yanayotumika kusafirishia maziwa yanatozwa utitiri wa kodi ambazo kwa kiasi kikubwa zinawakwamisha kufanya shughuli zenu, hivyo na hili tutaenda kuangalia," alisema.

Wakati Serikali ikiahidi kushughulikia changamoto hizo, Waziri Ndaki alizitaka TDB na TAMPA kuhakikisha zinapata suluhu ya changamoto ya kiwango kidogo cha matu-

**"Katika kuhakikisha tunawalinda wasindikaji na wazalishaji wa maziwa wa ndani, tutaendelea kutoza Sh2,000 kwa kila pakiti ya maziwa yanayoingia kutoka nje."**

Mashimba Ndaki

mizi ya bidhaa hiyo nchini.

Mwenyekiti wa TAMPA, Fabian Mwakatuma alisema moja ya tozo inayolalamikiwa na wasindikaji ni ile inayotozwa kwa magari ya kubebea maziwa kutoka sehemu moja kwenda nyine.

Magari hayo yamekuwa yakilazimika kufanya wa usajili kila mwaka na kulipiwa katika maeneo matatu tofauti ikiwemo TDB, Mamlaka ya viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Usafiri wa Ardhini (Latra) kwa Sh200,000 kila eneo.

Akichangia hoja katika mukutano huo, moja wa wasindikaji wa maziwa kutoka Siha mkoani Kilimanjaro, Hellen Usiri alisema mbali na uwepo wa utitiri wa tozo pia uwepo wa wauzaji maziwa wasio rasmi umekuwa changamoto kubwa.

## NIPASHIE UR 15



Mkurugenzi Mkazi wa Kampuni ya kimataifa ya kusafirisha mizigo ya DHL, Paulo Makolosi (kushoto) akimkabidhi Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Abdalla Ulega boti ya doria ya uvuvi kwenye hafla iliyofanyika mwishoni mwa wiki mkoani Kigoma. Kulia ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dk. Rashid Tamatamah. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**